Jarida la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania

# TARI HABARI

*Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo*

Toleo No. 03 | Januari - Machi 2026 | www.tari.go.tz




## WAZIRI MKUU AIKABIDHI TARI NDEGE NYUKI ILI KUIMARISHA UTAFITI

## KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA MAFANIKIO YA MRADI WA UMWAGILIAJI TARI HOMBOLO



# UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU


## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
DKT. THOMAS BWANA
Mkurugenzi Mkuu TARI

**KATIBU**
DKT. SOPHIA KASHENGE
Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia, Biashara na Mahusiano

**WAJUMBE**
EVELYNE MPASHA
Kaimu Meneja Menejimenti ya Maarifa na Mawasiliano

DKT. RAJAB KANGILE
Kaimu Meneja wa uhaulishaji wa teknolojia, uendeshaji wa biashara na ushirikiano

DKT. ABDULLAH MKIGA
Kaimu Meneja wa Kituo, TARI Kifyulilo

DKT. ANDEKILILE MWAMAHONJE
Mtafiti Mwandamizi

DEODATUS KIRIBA
Mtafiti Mwandamizi

**WAANDISHI**
MUGINI SINGIRA
Afisa Uhusiano kwa Umma

GERALD USIRI
Afisa Uhusiano kwa Umma

MARIA PAUL
Afisa Uhusiano kwa Umma

HOSEA R. BILATANGUYE
Afisa Uhusiano kwa Umma

TariTanzania | Tanzaniatari | official_taritanzania | TARI Tanzania | TARI


**Ndugu msomaji na mdau wa sekta ya kilimo,**

Napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa dhati kwa ushirikiano wenu endelevu katika kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kutekeleza wajibu wake wa msingi. TARI ina jukumu la kufanya tafiti zinazotatua changamoto halisi za wakulima, hususan katika maeneo ya mbegu, afya ya udongo na utoaji wa mafunzo ya kilimo bora pamoja na kushauri watunga sera katika sekta ya kilimo.

Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka (Januari–Machi), Taasisi imeendelea kuimarisha mchango wake katika kukuza tija ya kilimo na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa kupitia tafiti na ubunifu wa teknolojia mbalimbali. Katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, TARI inaendelea kutekeleza mradi wa umwagiliaji wa hekta 838.5 wenye thamani ya shilingi bilioni 17.8 ulioanza tarehe 16 Mei 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Disemba 2026. Mradi huu unatekelezwa katika vituo 11 vya TARI.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha kazi za utafiti wa kilimo kwa kuwezesha majaribio kufanyika kwa kipindi cha mwaka mzima na pia kutawezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora za madaraja mbalimbali kwa kipindi cha mwaka mzima.

Aidha, mradi huo pia utasaidia kuvutia ushirikiano na uwekezaji wa wadau katika shughuli za utafiti na uzalishaji wa mbegu.

Mpendwa msomaji, hadi kufikia Februari 2026, TARI imeendelea kupata mafanikio makubwa katika utafiti ambapo aina 16 za mbegu, za migomba (14) na muhogo (2) zipo katika hatua za kuidhinishwa, na aina 28 za mazao mbalimbali zimewasilishwa TOSCI kwa majaribio



*DKT. THOMAS BWANA*
*MKURUGENZI MKUU - TARI*

ya utambuzi na umahiri.

Taasisi pia imechambua zaidi ya sampuli 4,000 za udongo na kutoa mapendekezo sahihi ya matumizi ya mbolea kwa wakulima. Katika kuendeleza utafiti, vinasaba zaidi ya 33,000 vimehifadhiwa, huku tafiti za mazao ya kakao, karanga na tende zikiendelea kuimarishwa.

Katika mfululizo wa toleo la Jarida la TARI Habari, tutaendelea kuainisha jitihada tunazozifanya katika utafiti na kutoa matokeo yake kwa wakulima na wadau wa kilimo ili kuonyesha dhamira ya TARI katika kuendeleza kilimo chenye tija, kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi na kinacho chochea ukuaji wa uchumi wa taifa na kuchangia usalama wa chakula pamoja na kuongeza kipato cha wakulima.

Nakusihi mpendwa msomaji uendelee kutufuatilia na pindi utakapokuwa unahitaji msaada wowote ama ushauri usisite kuwasiliana nasi ili tuweze kukupa majibu ya changamoto uliyonayo katika sekta ya kilimo.

***TARI-UTAFITI KWA MAENDELEO YA KILIMO***




# WAZIRI MKUU AIKABIDHI TARI NDEGE NYUKI ILI KUIMARISHA UTAFITI NA KUHIMIZA MATUMIZI ENDELEVU YA ZANA ZA KILIMO

**WAZIRI** Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb) ameikabidhi Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ndege nyuki (Drone) ikiwa ni moja ya zana za kilimo ili kuongeza ufanisi katika tafiti mbali mbali za kilimo.

Mhe. Dkt. Nchemba amekabidhi ndege nyuki (drone) hiyo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Afrika kuhusu Matumizi endelevu ya Zana za Kilimo (Africa Conference on Sustainable Agricultural Mechanization - ACSAM) uliofanyika Jijini Dar es Salaam Februari 3 – 6, 2026. Hii ni mara ya kwanza kwa Mkutano huo ambao umeratibiwa na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) kufanyika nchini Tanzania.

Ndege Nyuki hiyo ilikabidhiwa kwa Kituo cha TARI Naliendele kilichopo Mkoani Mtwara kwa ajili ya kutumika kunyunyuzia viuatilifu kwenye zao la korosho katika msimu wa kilimo unaoanza Mwezi Aprili, 2026.

Awali, katika taarifa yake wakati wa ufunguzi wa Mkutano huo ambao pia ulihudhuriwa na Mawaziri wa Kilimo kutoka nchi za Nigeria, Somalia, Niger, Afrika ya Kati, Rwanda na Senegal, Waziri wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo alibainisha kuwa Mkutano huu pamoja na mambo mengine utajadili masuala mbalimbali kuhusu zana za kilimo pamoja na kupata uzoefu wa masuala mbalimbali yanayohusu namna bora ya kuimarisha matumizi ya zana za kilimo kupitia matumizi ya teknolojia za kisasa zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Chongolo ameongeza kuwa mkutano huu pia umewakutanisha pamoja Watunga Sera, Wawakilishi wa Serikali, Wadau wa Maendeleo, Watafiti wakiwemo wa TARI, Wakulima, Asasi za Kiraia na Mashirika ya Sekta binafsi yanayojihusisha na maendeleo ya vijijini na uendelezaji wa Sekta ya Kilimo ili kupeana uelewa wa namna bora ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Sekta ya Kilimo.

Mbali na ufunguzi wa Mkutano huo, Mhe. Dkt. Nchemba pia amezindua rasmi Mkakati wa Taifa wa Zana za Kilimo wa Awamu ya Pili (2026 hadi 2035) ambao umelenga kuimarisha matumizi, utengenezaji na uendelezaji wa zana za kilimo.



# KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA MAFANIKIO YA MRADI WA UMWAGILIAJI TARI

**KAMATI** ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa utekelezaji wa shughuli za Utafiti pamoja na usimamizi wa mradi wa umwagiliaji wa mashamba ya mbegu.

Pongezi hizo zimetolewa Machi 18, 2026 wakati Kamati hiyo ya Bunge ilipotembelea Kituo cha TARI Hombolo kilichopo Jijini Dodoma kukagua maendeleo ya miradi wa Umwagiliaji na kujionea shughuli mbalimbali za utafiti kituoni hapo.

Miongoni mwa miradi waliyokagua ni ukarabati wa mabwawa na mradi wa utafiti wa kilimo cha tende, miradi ambayo inalenga kuongeza uzalishaji wa mbegu, kuendeleza shughuli za utafiti hata wakati wa kiangazi na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika aliipongeza TARI kwa usimamizi mzuri wa miradi hiyo na kueleza kuridhishwa na hatua zilizofikiwa katika miradi hiyo.

*"Nawapongeza TARI kwa kusimamia kazi nzima ya umwagiliaji wa mashamba ya mbegu. Kazi iliyofanyika ni kubwa, tumeona maji, pump house na sehemu mnayochukulia maji. Tumetembelea mashamba na kwa ujumla tumeridhika na kiwango mlichofikia" alisema Mhe. Mwanyika.*

Mhe. Mwanyika aliongeza kuwa Kamati itapata nafasi wakati mwingine kuja kuangalia ukamilifu wa mradi huo na kuona mashine zinavyomwagilia mashamba ya mbegu.

Kwa upande wake, Mjumbe wa kamati hiyo ambaye pia ni Mbunge wa Mvumi Mhe. Livingstone Lusinde alisisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi mbalimbali, kuongeza ubia na sekta binafsi katika usambazaji wa mbegu bora, pamoja na kudhibiti mbegu feki sokoni ili kuongeza tija katika sekta ya kilimo.

Awali katika taarifa yake, Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alieleza kuwa kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya Utafiti yanayosimamiwa na Kituo cha TARI Hombolo kutaongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu kutoka tani 15 hadi tani 50 kwa mwaka na kusaidia wananchi kupata mbegu bora kwa haraka.



Aliongeza kuwa shughuli za utafiti na uzalishaji wa mbegu Kituoni hapo zimekuwa zikiathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukame, hivyo mradi huu ni ishara ya mapinduzi yanayoendelea katika sekta ya kilimo, hususan katika kuboresha shughuli za utafiti, kuongeza uzalishaji wa mbegu zenye tija kwa wakulima.

***"Nia yetu ni kubuni teknolojia zinazotoa suluhisho la moja kwa moja kwa changamoto za wananchi, huku tukizingatia mnyororo mzima wa thamani kuanzia afya ya udongo hadi masoko, tukielekea kufikia Dira 2050," alisema Dkt. Bwana.***

Katika hatua nyingine, Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilipata fursa ya kutembelea maonyesho ya teknolojia mbalimbali za mbegu pamoja na mradi wa kilimo cha tende, zao lenye thamani kubwa kiuchumi, unaolenga kuwapatia wakulima mbadala wa biashara pale mazao ya chakula yanaposhindwa kutokana na ukame, pamoja na kuongeza kipato cha kaya.



# OFISI YA MAKAO MAKUU YA TARI MTUMBA KUKAMILIKA FEBRUARI, 2027

**UJENZI** wa Ofisi ya Makao Makuu ya TARI katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma ulioanza mapema mwezi Februari, 2026 unatarajia kukamilika Februari, 2027 chini ya Mkandarasi Pioneers Builders Ltd.

Awali akiongelea kuhusiana na mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya TARI, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo (Umwagiliaji na Zana za Kilimo), Mhe. Mhandisi Athumani J. Kilundumya, ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kuhakikisha ujenzi wa jengo jipya la utawala unakamilika ndani ya muda uliopangwa.

Mhe. Mhandisi Kilundumya alitoa agizo hilo tarehe 9 Januari, 2026, wakati alipotembelea Ofisi za TARI Jijini Dodoma na kueleza kuwa Wizara tayari imepata fedha za kutosha kwa ajili ya mradi huo, hivyo hakuna sababu za kuchelewesha utekelezaji wake.

***"Wizara imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi huu. Niagize TARI kuhakikisha inafanya uchaguzi wa wahandisi wenye ujuzi na kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa pamoja na kukamilisha ujenzi ndani ya miezi sita bila ucheleweshaji wowote", alisisitiza Nhe. Mhandisi Kilundumya."***

Katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu alipata fursa ya kutembelea idara mbalimbali na alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana kwa utendaji wake, akibainisha kuwa TARI imekuwa kioo cha Wizara ya Kilimo kupitia kazi zake za utafiti ambazo zimekuwa zikigusa na kuimarisha maisha ya Watanzania wengi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, aliishukuru Wizara ya Kilimo kwa msaada wake wa kudumu, hususan katika uboreshaji wa miundombinu na kuongeza kuwa Wizara imetoa takribani shilingi bilioni 1.5 ambazo zimeelekezwa katika kutatua changamoto mbalimbali za watumishi wa taasisi hiyo kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Kwa sasa Ofisi za Makao Makuu ya TARI yapo katika Kituo cha TARI Makutupora na pindi ujenzi ukikamilika watumishi wote wa TARI Makao Makuu watahamia Ofisi mpya katika eneo la Mtumba.

## DIRA & DHIMA

**DIRA; Kuwa Kituo cha Kimataifa cha ubora katika utafiti wa kilimo kwa maendeleo endelevu.**
**DHIMA; Kuendeleza, kusambaza na kutoa mwongozo wa kisera kuhusu teknolojia zinazofaa za kilimo ili kuboresha maisha ya wananchi.**



# CHONGOLO AFUNGUA MKUTANO WA TATHMINI WA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2025/2026

**WAZIRI** wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo (Mb) amesema dhamira ya Serikali katika zao la Korosho imelenga kuongeza uzalishaji wa Korosho ghafi hadi kufikia tani 1,000,000 na kuwezesha ubanguaji kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2029/2030.

Mhe. Chongolo alibainisha hayo wakati akifungua kikao cha tathmini ya uzalishaji, masoko na ubanguaji wa Korosho msimu wa 2025/2026 na mpango wa maandalizi ya msimu wa 2026/2027, kilichofanyika Aprili 14, 2026 katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF Jijini Dodoma.

Ameongeza kuwa uzalishaji wa zao hilo umeongezeka kwa miaka mitatu mfululizo ndani ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu kutoka tani 310,787 msimu wa 2023/2024 hadi tani 618,497 msimu wa 2025/2026, ongezeko ambalo linatokana na ubanguaji kupitia mradi mkubwa wa kongani la viwanda vya kubangua korosho mkoani Mtwara na ongezeko kubwa la upandaji wa miche bora ya mikorosho ambapo katika msimu huu miche 4,220,000 imeshapandwa.

Alieleza kuwa ongezeko la uzalishaji katika zao la Korosho umewezesha Tanzania kuwa mwenyeji mtarajiwa wa Jukwaa la Dunia la Wadau wa Korosho (World Cashew Conference) linalotarajiwa kufanyika mapema mwaka 2027, Jijini Dar es Salaam.



Mbinu ya uzalishaji korosho kwa njia tishu

Awali akiwasilisha salam kutoka TARI kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Naliendele Dkt. Geradina Mzena alielezea shughuli zinazofanywa na taasisi katika tasnia ya korosho na mikakati ya utafiti kwa msimu ujao wa 2026/2027 ambazo ni Utafiti, Uzalishaji mbegu na miche, uhaulishaji wa teknolojia za utafiti kwa maafisa Ugani, wakulima na wadau, shughuli za Miradi na jitihada nyingine ikiwamo matokeo ya utafiti wa mbolea za majani kwenye zao la korosho na programu ya "Beyond Cashew Crop (BCC)" kwa kuendesha zao la Korosho sanjali na mazao mengine.



*Dkt. Geradina Mzena, Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Naliendele*

Wajumbe washiriki wa mkutano huo walipongeza jitihada zinazofanywa na TARI na wadau wengine katika tasnia ya Korosho na kuomba kuongeza juhudi zaidi ili kuhakisha tija na uzalishaji vinaongezeka hadi kufikia tani 1,000,000 ya uzalishaji nchini ifikapo msimu wa 2029/2030.

Aidha, wadau hao wameiomba Serikali kuwekeza zaidi kwenye tafiti za zao la Korosho ili kuongeza uzalishaji wa mbegu na miche inayokabiliana na mabadiliko ya tabianchi na visumbufu vya mimea na kuongeza usambazaji wa pembejeo kwa wakati na mizani ya kidigitali, ikiwa ni pamoja na kuongeza huduma za ugani.




# TARI YASHIRIKI KIKAO CHA PAMOJA CHA MAANDALIZI YA MKUTANO WA DUNIA WA KOROSHO (WORLD CASHEW CONFERENCE) 2027

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeshiriki katika kikao cha pamoja cha maandalizi ya Mkutano wa Dunia wa Korosho (World Cashew Conference) 2027 kilichofanyika Februari 4, 2026 Jijini Dar es Salam ambapo Tanzania itakuwa Mwenyeji wa Mkutano huo.

Mkutano huo wa Dunia wa Korosho ambao unatarajiwa kufanyika nchini Tanzania Januari 20 – 24, 2027 pamoja na mambo mengine utajadili fursa na changamoto zilizopo kwenye tasnia ya Korosho ili kuimarisha na kukuza tasnia ya zao hilo kwa manufaa ya wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani pamoja na kujengeana uwezo.

Kikao hicho cha kwanza cha maandalizi kimehudhuriwa na viongozi kutoka World Cashew Conference ambao ni Bw. Srivatsava G na Bw. Vinayak Maharwade ambao wote ni Wakurugenzi wa Eventell Global. Kwa upande wa TARI, ujumbe uliongozwa na Dkt. Sophia Kashenge ambaye ni Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknoloji na Mahusiano na Dkt. Wilsoni Nene (CRI) kutoka Kituo cha TARI Naliendele. Wengine ni William Mbasa, Gaspar Mgimiloko kutoka TARI Naliendele na Rose Kaguo kutoka TARI Mikocheni.



Mbinu ya ubebeshaji wa mikorosho mikubwa kuboresha uzalishaji



Akiongoza kikao hicho, Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) Bw. Godfrey Malekano alisema hii ni fursa kubwa sana kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano huo wa WCC 2027 ambao unatarajiwa kufanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwl. Julius Kambarage Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Kituo cha TARI Naliendele ni mahususi kwa ajili ya utafiti na uendelezaji wa zao la korosho nchini.



# CHONGOLO AZITAKA TAASISI ZA WIZARA YA KILIMO KUWA WABUNIFU NA KUFANYA KAZI KWA UADILIFU

**WAZIRI** wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo (Mb) ameziagiza Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa uadilifu ili kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo na kuhakikisha sekta ya kilimo inaendelea kuaminika kama mhimili mkuu wa uchumi wa taifa na kukifanya kilimo kuwa na mvuto kwa wengine kuwekeza.

Mhe. Chongolo ametoa agizo hilo April 10, 2026 katika ukumbi wa Mikutano wa Kilimo IV wakati wa Kikao kazi na Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi na Menejimenti za Taasisi zilizochini ya Wizara ya Kilimo ambazo ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa mbegu Tanzania (TOSCI) pamoja na Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kujadili utekelezaji wa mikakati mbalimbali waliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kuangalia mwelekeo wa bajeti na mikakati ya mwaka ujao wa fedha 2026/2027.

Amezitaka Taasisi hizo kuondoa mizigo kwa viongozi na kuwajibika ipasavyo katika kuleta matokeo yenye tija kwa wakulima huku akitaka kuimarishwa kwa uratibu, uwajibikaji na matumizi ya teknolojia katika kuleta ushindani kwa manufaa ya wakulima na taifa kwa ujumla huku akihimiza Taasisi hizo kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu kazi zao.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde (Mb) amewasisitiza Wakuu wa Taasisi kusimamia vizuri taasisi zao na kuhakikisha wanakabiliana na kila aina ya ubadhirifu na ukiukwaji wa maadili ya kazi ili kuendelea kujenga na kuimarisha taswira na kazi nzuri zinazofanywa na taasisi.


Awali, akiwasilisha utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya TARI kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kuangalia mwelekeo wa bajeti na mikakati ya mwaka ujao wa fedha 2026/2027, Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alibainisha kuwa hadi kufikia Februari, 2026 TARI imetumia kiasi cha shilingi 4,621, 052, 603/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya utafiti, uhaulishaji teknolojia na uzalishaji wa mbegu huku kiasi cha shilingi 318, 524,081/= zikiwa katika mpango wa utekelezaji hadi kufikia Juni, 2026.

Kuhusu mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Dkt. Bwana ameomba kuidhinishiwa na Wizara ya Kilimo kiasi cha shilingi bilioni 130.8 ikiwa ni bajeti ya TARI kwa mwaka mzima, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 38.7 sawa na asilimia 29.59% ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 92.1 sawa na asilimia 70.41% ni fedha za maendeleo.

Taasisi za TOSCI, TFC pamoja na CPB nazo ziliwasilisha utekelezaji wa bajeti wa taasisi zao kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na mwelekeo wa bajeti na mikakati ya mwaka ujao wa fedha 2026/2027.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde (Mb), Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Umwagiliaji na Zana za Kilimo, Mhandisi Athuman Kilundumya, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula, Prof. Peter Msoffe pamoja na Menejimenti ya Wizara ya Kilimo.





# TARI YASHIRIKI MKUTANO WA 4 WA KIKANDA WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU-EAC 2026

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeshiriki katika mkutano wa nne wa kikanda wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ( 4th EAC Regional Science, Technology and Innovation Conference) Jijini Kigali, Rwanda.

Mkutano huu ulioanza tarehe 31 Machi, 2026 - tarehe 1 April, 2026 ulilenga kuhimiza matumizi ya Akili Unde (AI) katika kuchochea maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.


Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa Mkutano huo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Thabit Kombo, alihimiza wataalam kutoka Tanzania na Afrika Mashariki kuwa wabunifu na wavumbuzi wa teknolojia zinazotatua changamoto halisi za jamii, badala ya kuwa watumiaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi.

TARI ikiiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Dkt. Thomas Bwana ilipata fursa ya kubadilishana uzoefu na wadau wa Kikanda na Kimataifa na kujadili nafasi ya Akili Unde (AI) katika kuboresha tafiti za kilimo, kuongeza tija na kuimarisha mifumo ya uzalishaji na masoko ya mazao.

Mkutano huu pia ulihudhuriwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb), Balozi wa Tanzania nchini Rwanda, Mhe. Dkt. Habib Kambanga pamoja na viongozi mbalimbali wa taasisi, mashirika na asasi za kiraia kutoka Tanzania.

Kufanyika kwa Mkutano huu ni hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika kukuza teknolojia bunifu katika mageuzi ya kilimo, sayansi na teknolojia kwa ujumla.






# SERIKALI KUIMARISHA MASOKO KWA ZAO LA PAMBA

**WAZIRI** wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo (Mb), amesema Serikali itaendeleza jitihada za kuimarisha zao la Pamba kwa kutoa elimu na pembejeo kwa wakulima ili kuleta tija na bei yenye uhalisia na kuongeza thamani ya zao hilo kupitia usindikaji wa ndani na kuimarisha masoko ya uhakika kwa wakulima katika mnyororo mzima wa thamani wa zao hilo.

Mhe. Chongolo ametoa kauli hiyo wakati akifungua Mkutano wa Wadau wa tasnia ya zao la pamba tarehe 16 Aprili 2026, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma na kuwataka wadau wa tasnia ya pamba kuongeza uzalishaji na kuhakikisha pamba inayozalishwa nchini inachakatwa hapahapa ili kuongeza ajira na pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mkutano huo uliowakutanisha viongozi wa Serikali, Wataalamu wa kilimo pamoja na wakulima kutoka maeneo mbalimbali nchini waliojadili changamoto na fursa zilizopo katika sekta hiyo.

Akizungumzia kuhusu ushirikiano, Mhe. Chongolo alieleza kuwa Serikali inafanya kazi kwa kushirikiana na Sekta binafsi ili kuvutia uwekezaji



katika mnyororo mzima wa thamani wa zao la pamba kuanzia shambani hadi viwandani na kuwataka wadau wote wa zao la pamba kushirikiana ili kutatua changamoto zilizopo ili kufikia malengo ya kuongeza tija na kuinua maisha ya wakulima.

Ameongeza kuwa, uwekezaji katika viwanda vya nguo na usindikaji wa pamba utasaidia kupunguza utegemezi wa soko la nje ambalo limekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya bei hatua ambayo itaongeza ushindani wa pamba ya Tanzania katika soko la Kimataifa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba (TCB) Christopher Gachuma alieleza kuwa changamoto ya bei ndogo ya zao la pamba inachangiwa kwa kiasi kikubwa na utegemezi wa soko la Kimataifa na kuishauri Serikali kuongeza uwekezaji katika viwanda vya ndani vinavyochakata pamba ili kupunguza utegemezi huo na kuongeza thamani ya zao hilo.

Kituo cha TARI Ukiriguru kilichopo Mkoani Mwanza ni Kituo chenye jukumu mahsusi la kufanya utafiti wa zao la pamba nchini na kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa zao hilo katika mnyororo wa thamani ili kuongeza tija ya zao hilo.



# KIJUE KITUO CHA TARI KIFYULILO



**TARI** KIFYULILO ni mojawapo ya vituo vya utafiti vilivyo chini ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI). Kituo hiki kipo katika Wilaya ya Mufindi, Mkoa wa Iringa. Kituo kikuu kipo umbali wa takriban kilomita 60 kutoka mji wa Mafinga na kilomita 150 kutoka Manispaa ya Iringa.

Kituo hiki kilianzishwa awali kama shamba la chai, ambapo miundombinu yake ilinunuliwa mwaka 1986 kutoka kwa raia wa Ujerumani kwa lengo la kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Chai. Mwaka 1998, mamlaka ya kituo yalipanuliwa na kufanya tafiti kwenye mazao ya maharage, viazi mviringo, na mahindi, pamoja na utafiti wa nyongeza juu ya ngano na mazao ya bustani

Kituo hiki kina eneo la hekta 220 na kati ya hizo, hekta 68 ni mashamba ya majaribio, mashamba ya mfano na mashamba ya uzalishaji wa chai. Eneo lililobaki lina uoto wa asili, miti ya kupanda, Barabara na majengo.

**TARI Kifyulilo ina vituo vidogo viwili:**

I). Seatondale: Hiki ni kituo kilichopo Manispaa ya Iringa. Kituo kina eneo la Hekta 11.3 ambapo eneo la ekari 4.6 linatumika kwa majaribio na mashamba ya mfano na kinategemea kuongeza hekta 1.6 kwa shughuli hiyo baada ya kutengeneza mtaro wa kuzuia maji kujaa kwenye mashamba. Eneo lililobaki lina uoto wa asili, barabara na majengo. Kituo kipo mkabala na kituo cha mabasi cha Ipogolo njia kuu ya kutoka Dar es Salaam kuelekea Mbeya na Njombe.

II) Isimani: Ni kituo kilichopo Halmashauri ya Iringa vijijini. Kituo hiki kimewekwa kimkakati katika Kanda kuu za usafirishaji zinazounganisha Dodoma na mikoa ya Mbeya na Njombe.

Kituo kina jumla ya eneo la Hekta 100. Hekta 80 zinafaa kwa mashamba ya majaribio na mashamba ya mfano. Eneo linalobaki lina uoto wa asili, Barabara na majengo. Kituo kinajishughulisha na uzalishaji wa mbegu za maharage, soya na mazao mengine.



*Jengo la Kituo kidogo cha Isimani*



*Shamba la mfano la kilimo cha kabichi kwenye kituo kidogo cha Seatondale*



# TARI YAHIMIZA MATUMIZI YA ZANA ZA KILIMO NA KILIMO SHADIDI CHA MPUNGA ILI KUONGEZA TIJA

**WATAFITI** kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) wamehimiza matumizi ya zana za kisasa za kilimo katika zao la Mpunga yanayoambatana na teknolojia ya kilimo Shadidi cha Mpunga ili kuongeza tija kwa Wakulima.

Wito huo umetolewa Machi 09, 2026 na Mtafiti Mwandamizi kutoka TARI Ifakara Dkt. Kulwa Furahisha (kwa niaba ya mratibu wa mradi Dkt. Atugonza Bilaro) wakati wa siku ya Mkulima iliyofanyika kituo cha TARI Dakawa na katika Skimu ya Mpunga ya Ilonga iliyopo Kilosa Mkoani Morogoro ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kilimo shadidi cha Mpunga (SRI).

Dkt. Furahisha amesema kilimo shadidi cha Mpunga kinamwezesha Mkulima kutumia mbegu kidogo wastani wa kilogram 3 hadi 5 kwa ekari tofauti na kilogramu 20 kwa ekari katika kilimo cha kawaida, pia kinawezesha matumizi ya maji kidogo huku mavuno yakiongezeka kulinganisha na kilimo cha kawaida.



Katika kueneza teknolojia hiyo Dkt. Furahisha amesema TARI imetoa mafunzo kwa wakulima wa mpunga katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Chalinze Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara, Wilaya ya Kilombero na Kilosa Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Iringa Mkoa wa Iringa pamoja na Wilaya ya Mbarali katika Mkoa wa Mbeya.

Katika kuendelea kupunguza gharama za uzalishaji na ugumu wa shughuli za shamba pamoja na zana zingine, kilimo shadidi kinahimiza matumizi ya vipalizi ambavyo vinarahisisha zoezi la palizi.

Pamoja na hiyo, Kufuatia teknolojia ya kitalu mkeka ambayo inawezesha kupanda miche michanga iliyokaa kwenye kitalu siku 8-14 tangu kuanza kuota, Dkt. Furahisha amesema katika siku ya Mkulima, wametoa mafunzo ya matumizi ya zana ya kupandia kwa mraba, hatua ambazo zinarahisisha zoezi la kupanda, zinapunguza gharama na kuwezesha matumizi ya vipalizi.

Kwa upande wake Mkulima wa Mpunga Skimu ya Ilonga Bwana Godfrey Paschal amesema tangu apate elimu kutoka TARI kuhusu kilimo shadidi cha Mpunga kwa kutumia teknolojia ya kitalu Mkeka ameongeza mavuno kufikia wastani wa gunia 30 kwa ekari tofauti na kilimo cha kawaida alichokuwa akivuna gunia 8-12.




# WAKULIMA WADOGO 1065 WANUFAIKA NA MAFUNZO YA UKUZAJI UJUZI KUTOKA TARI

**ZAIDI** ya wakulima wadogo 1065 kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Mbeya na Iringa wamenufaika na elimu ya kuongeza ujuzi na usindikaji wa mazao ya zabibu, alizeti, parachichi, nyanya na mchicha lishe kutoka kwa wakufunzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia uwezeshaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano.

Kati ya wakulima hao, wakulima 261 kutoka mkoani Dodoma walipata ujuzi na elimu ya usindikaji wa zao la zabibu, 258 kutoka mkoa wa Singida walipata ujuzi na elimu ya kilimo bora cha alizeti pamoja na usindikaji wa zao hilo, wakulima 266 kutoka mkoani Mbeya walipata elimu ya usindikaji wa zao la parachichi na wakulima 250 kutoka mkoani Iringa walipata ujuzi na elimu ya usindikaji wa mazao ya nyanya na mchicha lishe.

Awali, akifunga rasmi mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa wakulima na wasindikaji wadogo Januari 23, 2025 Mkoani Iringa, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Rahma Kisuo aliwapongeza na kuwashukuru TARI kwa kutoa mafunzo kwa wakulima wa mikoa hiyo minne na kuongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kutekeleza mkakati wa kuwawezesha wakulima na wasindikaji wadogo kwa kuwapatia ujuzi utakao wawezesha kuongeza ufanisi na tija na kuwaongezea uwezo wa kibiashara.

Mhe. Kisuo aliwataka washiriki wote waliohitimu mafunzo hayo kutumia elimu, ujuzi na maarifa waliyoyapata katika kujiimarisha zaidi katika kilimo na kujiongezea kipato kwenye bidhaa za usindikaji pamoja na kuwa mabalozi wazuri wa kupeleka elimu waliyoipata kwa jamii ili nao waweze kunufaika na elimu hiyo na kujikwamua kiuchumi kupitia elimu ya usindikaji.

***"Mkirudi kwenye maeneo yenu ya kazi mkawe mabalozi wa mabadiliko katika jamii pia wahitimu wote wa mafunzo wakulima na wasindikaji wadogo nawasihi mtumie vizuri elimu mliyoipata kutoka TARI ili kukuza, kuendeleza na kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya kilimo nchini" Amesema Mhe. Kisuo.***

Mh. Kisuo alitoa wito kwa wadau wa sekta ya Kilimo ndani na nje ya nchi kuendelea kushirikiana na Serikali ili kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo na kuifanya kuwa nguzo imara ya Uchumi nchini.

Akizungumzia mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Ukuzaji Ajira kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano Bwana Godwin Mpelumbe alieleza kuwa Serikali tangu mwezi Juni 2025 kupitia program hii imewezesha jumla ya watanzania 157,847 kunufaika na mafunzo ya Ukuzaji Ujuzi na katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetoa fedha kwa ajili ya programu ya kuongeza ujuzi kwa wakulima na wasindikaji Wadogo 1,065.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa (TARI) Dkt. Thomas Bwana. aliishukuru Serikali kwa kuiamini TARI kutoa mafunzo hayo kwa wakulima wadogo na wasindikaji nchini na kuahidi kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano katika fursa nyingine za kutoa elimu kwa wakulima na wajasiriamali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima na wasindikaji wadogo. wameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwa karibu na wakulima na kuwapatia mafunzo hayo na kuomba mafunzo ya namna hiyo yawe endelevu kwani yanawasaidia kuwaongezea ujuzi wa kuboresha uzalishaji wa mazao yao na kuwafanya wajiongezee kipato.

Mbali na kufunga mafunzo hayo, Mhe. Kisuo alitumia jukwaa hilo kuzindua rasmi Mwongozo wa Uratibu Mafunzo ya Kuongeza Ujuzi kwa wafanyakazi.



# TARI, WADAU WAJADILI MATUMIZI YA TEKNOLOJIA ZA KISASA KATIKA KILIMO CHA ZAO LA MPUNGA NCHINI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na Taasisi ya NIBIO walikutana katika Mkutano wa Tatu wa Mwaka Machi 13, 2026 katika Ukumbi wa St. Gaspar, jijini Dodoma ambapo Pamoja na mambo mengine walijadili mafanikio yaliyopatikana katika zao la mpunga pamoja na kuweka mikakati ya kuendeleza matumizi ya teknolojia za kisasa katika kilimo cha zao hilo nchini.

Akifungua Mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana alieleza kuwa kuwa zao la mpunga lina nafasi muhimu katika kukuza ajira kupitia mnyororo wake wa thamani na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa hivyo matumizi ya teknolojia sahihi na za kisasa za kilimo ni muhimu katika kuongeza tija kwa wakulima.

Dkt. Bwana aliongeza kuwa tafiti zinazofanywa na TARI zina lengo la kuleta mageuzi chanya katika sekta ya kilimo hasa katika uzalishaji wa zao la mpunga na kuchangia kufikia malengo ya DIRA 2050.

Wadau wa Mkutano huo kwa pamoja walipokea matokeo ya Mradi wa Mifumo ya Kuimarisha uzalishaji wa zao la mpunga kupitia mradi wa kilimo shadidi (SRI) unaotekelezwa kwa pamoja kati ya TARI na ufadhili wa Serikali ya Norway.



Akiongelea kuhusu mradi wa kilimo shadidi (SRI) kwa upande wa Tanzania, Dkt.Udaya Sekhar kutoka Taasisi ya NIBIO alieleza kuwa utekelezaji wa mradi huo ulilenga kuboresha maisha ya wakulima wadogo wa mpunga kwa kuongeza uzalishaji huku ukipunguza athari kwa mazingira.

Aliongeza kuwa, kupitia mradi huo wakulima walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mpunga, matumizi ya kanuni na mbinu husishi za kuthibiti wadudu waharibifu, huduma za afya ya mimea, teknolojia bunifu za za kupandia na palizi ya magugu pamoja na kuimarisha ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali maji kwa ajili ya kilimo cha mpunga.

Kwa upande wake, Mtafiti Kiongozi wa Mradi wa Kilimo Shadidi, Dkt. Atugonza Bilaro alieleza kuwa ushirikiano na ubia katika kueneza na kupanua matumizi ya teknolojia za mifumo ya kuimarisha uzalishaji wa zao la mpunga pamoja na matumizi ya Nyenzo bunifu za zana za kilimo zinazotengenezwa kwa malighafi zinazopatikana ndani ya nchi zina mchango mkubwa katika kuongeza tija, huku zikitoa fursa za ajira kwa vijana na wanawake.

Mmoja wa wakulima walionufaika na mradi huo wa kilimo shadidi, Bi. Anna Maganga alieleza kuwa kupitia mafunzo na ushirikiano uliotolewa na TARI ameweza kuongeza tija kwenye mazao, kuanzisha vikundi vya vijana vinavyojihusisha na kilimo cha mpunga pamoja na kuanzisha darasa ili kutoa mafunzo kwa vijana ili kuwajengea ujuzi na kuwapatia fursa za kitalu Mkeka na kujiajiri.

Bi. Maganga alitoa shukrani kwa TARI kwa msaada na mafunzo yaliyomwezesha yeye na wakulima wengine kupata mafanikio katika kilimo cha zao la mpunga.




# WAKULIMA WA DABALO WANUFAIKA NA ELIMU YA MBEGU BORA KUTOKA TARI

**WAKULIMA** wa Kata ya Dabalo, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma wamenufaika na elimu sahihi na upatikanaji wa mbegu bora kutoka TARI wakati wa Maonesho ya Mbegu yajulikanayo Seed Fair yaliyofanyika Wilayani Chamwino Januari 6, 2026.

Maonesho hayo ambayo yaliratibiwa na Wizara ya Kilimo chini ya Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) yalikuwa na lengo la kuwawezesha wakulima kupata na kutumia mbegu bora ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

Kupitia wataalamu wake, TARI ilitoa elimu ya kilimo bora kwa wakulima pamoja na elimu ya teknolojia ya mbegu za mazao jamii ya mikunde, mahindi na alizeti.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wenzake, mmoja wa wakulima Bwana Mathias Chizua, mkazi wa Dabalo, alisema kuwa maonesho hayo yamekuwa fursa muhimu kwao kwani yamewawezesha kupata mbegu bora kwa bei nafuu pamoja na elimu ya kilimo inayotolewa na wataalamu hao wa TARI, jambo litakalowasaidia kuongeza tija katika uzalishaji na kuinua kipato chao.

Maonesho hayo yaliyofanyika kwa siku tatu, kuanzia tarehe 6 hadi 8 Januari 2026, mbali na TARI pia yalihusisha taasisi mbalimbali ambazo Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI), Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), wauzaji wa pembejeo pamoja na wakulima kutoka maeneo mbalimbali.







# PROGRAMU YA MIFUMO HIMILIVU YA CHAKULA (TFSRP) YAENDESHA MAFUNZO YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA, MATUMIZI SAHIHI YA VIUATILIFU NA JINSIA KWA VITUO VYA TARI SELIAN NA TARI KIBAHA

**PROGRAMU** ya Mifumo Himilivu ya Chakula (TFSRP) inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo imetoa mafunzo maalum kuhusu utunzaji wa mazingira, matumizi sahihi ya viuatilifu na ujumuishwaji wa masuala ya kijinsia kwa watafiti, maafisa kilimo na watumishi wa kada mbalimbali katika vituo vya TARI Selian kilichopo Mkoani Arusha na TARI Kibaha kilichopo Mkoa wa Pwani..

Mafunzo hayo ambayo yalifanyika February 22 -23, 2026, yalihusisha watumishi wa Vituo hivyo wakiongozwa na Wakurugenzi Dkt. Caresma Chuwa (TARI Selian) na Dkt. Nessie Luambano (TARI Kibaha) huku lengo kuu likiwa ni kujenga uelewa juu ya utunzaji wa mazingira pamoja na matumizi sahihi ya viuatilifu, masuala ya Jinsi na ukatili wa kijinsia na namna bora ya kupokea na kushughulikia maoni, malalamiko na maswali yanayohusu Programu ya TFSRP.

Aidha, mafunzo hayo pia yalilenga kuhakikisha watekelezaji wote wa programu hiyo ya TFSRP wanazingatia miongozo na taratibu zilizowekwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa programu.

Mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo watumishi hao yalitolewa na Bi Anet Babu -TFSRP, Ndugu Mapunda John - Wizara ya Kilimo, Bi Tulizo Malavanu - Wizara ya Kilimo, Ndugu Deodatus Kiriba - TARI HQ na Ndugu Maneno Chidege - TPHPA kupitia Program ya mifumo himilivu ya chakula (TFSRP)

Wakufunzi hao kwa nyakati tofauti walibainisha kuwa tafiti zinazofanyika chini ya programu ya TFSRP zinahimizwa kuzingatia mifumo ya kitaifa ya usimamizi wa mazingira, kuhakikisha uwezeshwaji na ujumuishwaji wa kijinsia vinapewa kipaumbele, pamoja na kujenga utamaduni wa uwazi na uwajibikaji kupitia mifumo madhubuti ya kushughulikia malalamiko na maoni.

Aidha, mafunzo hayo yamelenga kuongeza tija katika kilimo kupitia kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (Climate Smart Agriculture), kuimarisha usalama wa chakula kupitia matumizi sahihi ya viuatilifu pamoja na ushirikishwaji kikamilifu wa jinsi zote katika kilimo ili kukuza uchumi wa taifa.




# WADAU KUTOKA CHUO CHA NDC WATEMBELEA TARI KUJIFUNZA

**UJUMBE** wa watu 7 kutoka Chuo cha Taifa cha Ulinzi Tanzania (NDC) ulitembelea Kituo cha TARI Ukiriguru kilichopo Mkoani Mwanza Januari 21, 2026 kwa lengo la kujifunza shughuli mbalimbali za Utafiti wa mazao mbalimbali zinazofanywa na watafiti wa Kituo hicho.

Ujumbe huo ulioongozwa na Brigedia Generali Method Kamugisha ulipokelewa na Kaimu Mkurugenzi wa kituo hicho Dkt. Shadrack Mbapila ambaye alitoa wasilisho fupi kuhusu shughuli za utafiti zinazofanywa kupitia miradi mbalimbali kituoni hapo.

Brig. Gen Kamugisha alibainisha kuwa matarajio ya ziara yao ni kujifunza teknolojia mbalimbali za mazao ambazo kwa sehemu kubwa zinachangia kwenye usalama na upatikanaji wa chakula nchini.

Wageni hao walipata fursa ya kutembelea vitalu nyumba vya uzalishaji wa mbegu za muhogo, viazi vitamu, pamba na maabara ya utambuzi wa magonjwa ya mimea. Pia walijionea bidhaa na teknolojia nyingine ambazo zinapatikana kituoni hapo ikiwemo Rafiki Planter.

Baada ya ziara hiyo fupi ya kujifunza, ujumbe huo ulionesha kufurahishwa na kazi zinazofanywa na watafiti na kuahidi Kwenda kutumia vizuri elimu waliyoipata ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula.



Push weeder-kifaa cha kupalilia mpunga cha kusukuma kwa mkono

# Kipalizi cha mkono cha kutoa magugu katika zao la mpunga

**KIPALIZI** hiki kinalenga kuongeza ushiriki wa wanaume kwenye palizi ya zao la mpunga kazi ambayo awali ilikuwa ikifanywa kwa kiasi kikubwa na wanawake tu. Kwa kutumia kipalizi hiki rafiki kwa mkulima, mtu mmoja anaweza kupalilia ekari moja hadi mbili kwa siku ambapo awali ilichukua siku nne hadi tano kwa mtu mmoja kupalilia na kutoa magugu katika ekari moja ya shamba la mpunga kwa kutumia mikono.

Kipalizi hiki kinasaidia kutifua udongo, kuruhusu hewa kupenya, kinasidia kuzika magugu na hivyo kuongeza rutuba ya udongo na kulifanya shamba lionekane safi.

TARI imeshagawa zaidi ya Vipalizi 140 katika skimu za umwagiliaji katika Wilaya za Bunda (Mara), Kilosa, Kilombero (Morogoro), Iringa Vijijini (Iringa) na Mbarali (Mbeya).

Vipalizi hivyo vimetolewa bure kwa wakulima wa zao la mpunga ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa SRI wa kilimo shadidi unaotekelezwa na TARI.

Mradi huo wa SRI unahamasisha matumizi ya nyezo rahisi na rafiki kwenye kilimo cha zao la mpunga ili kumsaidia mkulima kuongeza tija na kumpunguza muda wa kufanya kazi za mikono.

Aidha, kipalizi hiki ni fursa kwa vijana kwani wanaweza kutengeneza na kuviuza kwa wakulima kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini.

## LUGHA ZA KILIMO

### Maana ya neno "KIHISI" katika kilimo

Katika kilimo, kihisi (sensor) ni kifaa kinachotumika kupima au kugundua hali mbalimbali za shamba ili kumsaidia mkulima kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia taarifa halisi kutoka shambani. Kuna Kihisi cha unyevu wa udongo, kihisi cha joto, kihisi cha mvua, kihisi cha virutubisho katika udongo, kihisi cha upepo, n.k.




# SHIRIKISHENI VIJANA KATIKA TAFITI-DKT. BURIANI

**MKUU** wa Mkoa wa Tanga Mhe. Dkt. Batilda Buriani ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kushirikisha vijana katika tafiti wanazofanya ili kuwasaidia vijana wengi wapende na kushiriki katika kilimo na kupata teknolojia rahisi na rafiki ili waone matokeo chanya katika kilimo.

Mhe. Buriani alitoa agizo hilo wakati akifunga kikao cha siku mbili cha mapitio ya shughuli za utafiti zilizotekelezwa na vituo vya Mlingano, Mikocheni na Kibaha chini ya programu za ndani kwa mwaka wa fedha 2024/25 katika Ukumbi wa Pope John Paul II, Chumbageni Jijini Tanga na kuipongeza TARI kwa kazi kubwa inayofanya ya kubadilisha maisha ya wananchi kupitia tafiti zenye tija.





Kutokana na umuhimu wa utafiti kwa maendeleo ya kilimo, Dkt. Buriani alisema Mkoa wa Tanga umetenga ekari 1,000 katika Wilaya ya Mkinga kwa ajili ya kuongeza maeneo ya utafiti, uzalishaji wa mbegu za awali, na hifadhi ya vinasaba vya mbegu hizo na kutaka kuanzishwa kwa mashamba ya mfano na kutoa elimu ya uzalishaji wa uyoga na mbogamboga ndani ya Jiji la Tanga ili kufungua fursa za kiuchumi kwa wakazi wa mjini, hasa vijana.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, aliainisha baadhi ya changamoto zinazoikabili taasisi hiyo, ikiwemo uchakavu wa mitambo ya uzalishaji na uhaba wa ardhi ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora kwa kiwango kikubwa.

Akijibu changamoto hizo, Dkt. Buriani alibainisha kuwa mchakato wa kupata eneo lingine katika Wilaya ya Pangani unaendelea vyema, mbali na zile ekari 1000 zilizotengwa Wilayani Mkinga kwa ajili ya shughuli za utafiti wa mbegu.

Kama ishara ya kuunga mkono juhudi za Mkoa wa Tanga katika kilimo cha mazao ya kimkakati, Mkurugenzi Mkuu wa TARI alimkabidhi Dkt. Buriani miche bora 10,000 ya karafuu ili igawiwe kwa wakulima wa Wilaya za Muheza na Mkinga ambako zao hilo hustawi vizuri.

Kikao hicho kilichofanyika tarehe 07 – 08 Januari, 2026 na kuwakutanisha watafiti na wadau wa kilimo wapatao 70 wakiwemo Mkuu wa Wilaya ya Tanga Mhe. Dadi Kolimba, Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge Bwana Saddy Kambona, pamoja na viongozi waandamizi kutoka Makao Makuu ya TARI Dodoma kilitanguliwa na maonesho ya teknolojia mbalimbali zinazozalishwa na TARI, ikiwemo uzalishaji wa ramani za udongo kwa ajili ya kilimo cha kidijitali, uzalishaji wa miche bora kwa njia ya chupa (Tissue Culture), uzalishaji wa miche ya matunda, viungo na viazi vitamu pamoja na uongezaji thamani wa mazao kama nazi.



# WIZARA YA KILIMO YAIPONGEZA TARI KWA MAPINDUZI YA TEKNOLOJIA NA MBINU BORA ZA KILIMO

**KAIMU** Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bi. Upendo Mndeme, ameipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa mafanikio makubwa ya kugundua na kusambaza kwa wakulima zaidi ya teknolojia 121 zinazohusisha mazao 16 nchini.

Akizungumza tarehe 4 Januari 2026 katika Manispaa ya Morogoro wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha mapokeo na tathmini kuhusu matumizi ya teknolojia hizo (Adoption Study), Bi. Mndeme alisema kuwa ubunifu wa TARI umekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha kilimo hususani kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe kwa wananchi.

Ameeleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2025, TARI imefanikiwa kuzalisha mbegu bora za mazao mbalimbali ikiwemo mtama, mhogo, viazi vitamu, mbogamboga, karanga, mpunga na maharage. Vilevile, taasisi hiyo imebuni mbinu jumuishi za kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao, teknolojia za uvunaji wa maji, pamoja na zana za kilimo zinazozingatia masuala ya kijinsia.

Aidha, Bi. Mndeme amesisitiza kuwa tathmini hiyo ni muhimu katika kuiwezesha Wizara ya Kilimo na wadau wengine kubaini kiwango cha mapokeo, matumizi na manufaa ya teknolojia hizo kwa wakulima, sambamba na changamoto zinazokwamisha matumizi yake.

Ameongeza kuwa matokeo ya tathmini yatatumika kuboresha sera, kanzidata na mbinu bora za uhaulishaji wa teknolojia kwa lengo la kuendeleza sekta ya kilimo na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa.






# TARI, FAO ZAJIPANGA KUBORESHA UTAFITI WA KILIMO CHA TENDE

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) pamoja na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) wamejipanga kuboresha utafiti wa kilimo cha tende nchini ili kuleta mageuzi ya kilimo kwa kuhakikisha teknolojia na utafiti zinaenda sambamba na mahitaji halisi ya wakulima.

Hayo yamebainishwa Februari 20, 2026 katika warsha ya siku mbili ya uthibitisho wa mwongozo wa Mafunzo ya kilimo cha tende iliyofanyika katika ukumbi wa Mesuma Hotel Jijini Dodoma ikiwa na lengo la kupitia, kuboresha na kuthibitisha rasimu ya mwongozo wa mafunzo ya Kilimo cha Mtende nchini ili kujibu changamoto halisi zinazowakabili wakulima.

Awali akifungua warsha hiyo, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia na Uhusiano Dkt. Sophia Kashenge ameeleza kuwa ili kuleta tija katika kilimo cha tende, TARI itaendelea kufanya utafiti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kubaini mahitaji ya wakulima yakiwemo aina ya udongo, mifumo ya umwagiliaji, matumizi sahihi ya mbolea pamoja na namna ya kuongeza thamani ya zao hilo na matokeo ya utafiti huo yatasambazwa kwa wakulima.

Mwongozo uliothibitishwa utatumika kama nyenzo muhimu ya marejeo kwa wakulima na maafisa ugani, ukichochea kilimo endelevu cha tende na kusaidia kuongeza uzalishaji, ustahimilivu, na fursa za kipato katika mnyororo wa thamani wa zao la mtende nchini Tanzania, mpango ambao unaakisi dhamira endelevu ya TARI na FAO katika kuimarisha uwezo wa kitaalamu na kuhamasisha ubunifu wa kilimo kote nchini.



Warsha hiyo pia ilijikita katika kuhakikisha mwongozo unaendana na viwango na sera za kitaifa za kilimo ili kuhakikisha maelekezo yanayotolewa yanalingana na malengo mapana ya sekta ya kilimo pamoja na mfumo wa kisheria wa Tanzania ambapo washiriki walithibitisha maudhui ya mwisho ya mwongozo huo kuwa uko tayari kwa uchapishaji na usambazaji nchi nzima.

Warsha hiyo ambayo iliandaliwa na TARI kwa kushirikiana na FAO ilihudhuriwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Kilimo, TARI, FAO, Maafisa Ugani, Serikali za Mitaa, ASA, TOSSIC, TPHPA na TFRA.



# WATAFITI TARI NALIENDELE WAPATIWA MAFUNZO YA UTENGENEZAJI WA BIOCHAR KWA AJILI YA KUBORESHA AFYA YA UDONGO

**KATIKA** kuzingatia umuhimu wa kuboresha afya ya udongo na kuongeza uzalishaji katika mazo, watafiti wa Kituo cha TARI Naliendele wamepatiwa mafunzo maalumu kuhusu utengenezaji wa biochar itokanayo na mabaki ya mazao hususan mabibo ya korosho (cashew apple biochar).

Mafunzo hayo yalifunguliwa na Mkurugenzi wa kituo hicho Dkt.. Geradina Mzena ambaye alisisitiza zaidi umhimu wa mafunzo hayo katika kuwajengea uwezo watafiti kuhusu teknolojia ya kuzalisha na kutumia biochar kama njia mojawapo ya kuboresha rutuba na afya ya udongo.



Mafunzo hayo ambayo yametolewa na wataalam wenye uzoefu katika teknolojia hiyo yalihusisha nadharia na vitendo ambapo baada ya mafunzo watafiti wa Kituo cha TARI Naliendele wanatarajia kuendelea na tafiti zaidi na majaribio ya matumizi ya biochar shambani, ili kubaini manufaa yake katika kuongeza uzalishaji wa mazao hususan korosho.



HABARILEO JUMATATU MACHI 9, 2026 | MAKALA 9

# JamiiYETU

11 OLDUVAI GORGE; NYAYO ZA MABABU 'ZINAZOTEMBEA'

14 SERIKALI INAVYOENDELEA KUBORESHA MAJENGO YA HALMASHAURI

## Watafiti wanawake wanavyochangia kukuza kilimo Tanzania

Na Mugini Singira

TANZANIA ni nchi inayojitosheleza chakula kwa asilimia 128, hatua kubwa na muhimu kwa taifa lenye watu waliotambua kilimo kama uti wa mgongo tangu enzi.

Hiyo inadhihirika kutokana na mchango wa sekta ya kilimo nchini katika mnyororo mzima wa thamani, inapochangia asilimia 26.5 katika Pato la Taifa, asilimia 65.6 katika kutoa fursa za ajira na asilimia 65 ya malighafi ya viwanda.

Ukweli ni kuwa, huwezi kuzungumzia mafanikio ya kilimo nchini bila kutambua mchango wa wanawake katika mnyororo wa thamani wa kilimo kuanzia shambani katika hatua ya kulima, sokoni kuuza bidhaa na uongezaji thamani.

Upo usemi kwamba, "Kama hujafanya utafiti, huna haki ya kuzungumza", hivyo suala la utafiti linabaki kuwa ni muhimu kwenye kilimo ili kuendelea kufanya kilimo chenye tija zaidi.

Kwa muktadha wa Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2026 makala haya yanalenga kuelezea mchango wa wanawake watafiti wa kilimo katika kupatikana tija.

Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa Machi 8, kila mwaka. Kwa mujibu wa vyanzo vya kihistoria, kwa mara ya kwanza iliadhimishwa Machi 8, 1975 baada ya Umoja wa Mataifa (UN) kuridhia siku hiyo kutumika kama siku rasmi ya kuikumbusha dunia juu ya haki za wanawake.

Kitaifa maadhimisho mwaka huu yanafanyika mkoani Arusha yakiwa na Kaulimbiu: "Wanawake na Wasichana 2025; Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji."

Utafiti unabaki kuwa muhimu kutokana na athari hasi za mabadiliko ya tabianchi zilizokuwa zikijitokeza na kufanya watafiti wanawake kutokubaki nyuma katika utafiti na ugunduzi wa teknolojia mbalimbali kama zinavyobainishwa hapa.

Ugunduzi wa mbegu za mgomba

Grace Kindimba ni Mtafiti Mwandamizi wa Kilimo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Tengeru kilichopo Arusha. Mtafiti huyo ni msimamizi wa Kanda ya Arusha na Kilimanjaro.

Mwaka 2016 katika mradi uliolenga kuchochea uzalishaji wa aina bora za migomba, alishirikiana na watafiti wenzake kugundua aina mpya nne za migomba.

Aina hizo ni Tariban 1, Tariban 2, Tariban 3 na Tariban 4 zilizosajiliwa mwaka 2021.

Anasema aina hizo zina sifa kinzani dhidi ya magonjwa na wadudu waharibifu wa migomba, huku zikitoa mavuno mengi.

Kwa mujibu wa Grace, ugunduzi wa mbegu hizo ulichochewa na ongezeko la magonjwa na wadudu waliokuwa wakishambulia migomba ya asili.

Miongoni mwa magonjwa hayo anasema ni pamoja na sigatoka nyeusi na mnyauko fuzali ya migomba.

Kwa upande wa wadudu, anasema ni bungua wa migomba na minyoo ya migomba.

Kwa kutambua kuwa migomba ni zao linalokaa muda mrefu, yeye na watafiti wenzake wakaanza kutumia taaluma zao ili kupata aina mpya zitakazoongeza uzalishaji, huku zikiwa kinzani dhidi ya magonjwa na wadudu.

Grace anasema baada ya kugundua aina hizo mpya, walizalisha miche 30,000 na kugawia wakulima katika mikoa inayolima migomba ikiwamo ya Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Mbeya, Kagera na Zanzibar kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI).

Kutokana na ugunduzi huo, Grace anashauri wakulima wakiwa wanaanzisha mashamba mapya, wazingatie kupata na kutumia mbegu bora ili kuepuka magonjwa kutokana na matumizi ya mbegu.

Uzalishaji haraka wa mbegu za viazi vitamu

Viazi vitamu ni zao muhimu la chakula linalotumika mara kadhaa kama kinga ya njaa.

Limekuwa na mwitikio mkubwa kwa wakulimwa hususani mikoa ya Kanda ya Ziwa, mbali na kuwa chanzo cha mapato kwa wakulima na wafanyabiashara katika mnyororo wa thamani nchini.

Aidha, uwepo wa viazi lishe (vyenye vitamini A) unaongeza umuhimu wa zao hilo, hususani kwa watoto na wajawazito kukabiliana na changamoto za utapiamlo.

Kwa mujibu wa Mtafiti Mwandamizi wa Viazi Vitamu ambaye pia ni Meneja wa Kituo cha TARI Maruku, Dk Hadija Mussa Ally, uhaba wa mbegu bora na safi hususani mwanzoni mwa kipindi cha mvua ni miongoni mwa changamoto

Inaendelea uk.13

Meneja wa Kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) - Maruku, Dk Hadija Ally (kushoto) akitoa elimu kuhusu uchaguzi wa mbegu bora za viazi vitamu kwa wakulima katika Kituo cha Uhaulishaji wa Teknolojia kilichopo Nyakabindi mkoani Simiyu.








# TARI YATEMBELEA BODI YA MAENDELEO YA KILIMO NA RASILIMALI WANYAMA YA RWANDA (RAB)

**MKURUGENZI** Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana amefanya ziara nchini Rwanda kutembelea Bodi ya Maendeleo ya Kilimo na Rasilimali Wanyama ya Rwanda (RAB) na kukutana na viongozi wa Bodi hiyo akiwemo Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa RAB Dkt. Florence Uwamahoro.

Dkt. Bwana aliambatana na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu – DRI, Bw. Deodatus Kiriba pamoja na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia na Mahusiano – DTTP, Bw. Fikiri Stiliwati katika ziara hiyo ambayo ililenga kuanzisha ushirikiano wa kikanda katika utafiti na maendeleo ya kilimo kati ya TARI na RAB.

Katika mazungumzo yake, Dkt. Bwana alieleza maeneo mbalimbali ambayo TARI inatekeleza shughuli zake, pamoja na kuainisha maeneo muhimu ya ushirikiano kati ya TARI na RAB ili kuanzisha na kuimarisha mshikamano wa Kikanda hatua ambayo itaongeza kasi ya kuwafikia wadau wa ndani na nje ya nchi.

Miongoni mwa maeneo ya mashirikiano yaliyojadiliwa ni pamoja na utafiti wa mazao ya viazi mviringo, mpunga, ndizi, tufani, na zabibu.





# TARI, CHUO KIKUU CHA KILIMO SHANDONG CHA CHINA KUSHIRIKIANA KATIKA TAFITI, UBUNIFU WA TEKNOLOJIA NA KUBADILISHANA WATAALAMU

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imepokea ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Shandong katika ziara maalum iliyofanyika tarehe 14 Aprili 2026, jijini Dodoma, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kimkakati katika sekta ya kilimo.


Katika ziara hiyo, ujumbe huo ulitembelea vituo vya utafiti vya TARI Makutupora na TARI Hombolo ili kujionea shughuli za utafiti na uhaulishaji teknolojia zinazotekelezwa na TARI.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kukuza ubunifu na kuongeza tija katika kilimo. Naye Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu, Dkt. Deusdedith Mbanzibwa, alieleza maeneo ya kipaumbele ya ushirikiano ikiwemo bioinformatics, kubadilishana wataalamu, tafiti za pamoja na uhaulishaji wa teknolojia kwa wakulima.

Kwa upande wake, Rais wa Chuo Kikuu cha Shandong Prof. Leng Changjian, alieleza dhamira ya kuimarisha ushirikiano huo, akibainisha mafanikio ya China katika matumizi ya teknolojia za kisasa za kilimo.

Pande zote zimekubaliana kuendeleza ushirikiano katika tafiti, ubunifu wa teknolojia, kubadilishana wataalamu, pamoja na kuanzisha majukwaa ya pamoja ya utafiti hususan katika bayoteknolojia na molecular science.







# TARI YAANZA TATHIMINI YA MAPOKEO NA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA ZA KILIMO KUPITIA MRADI WA TFSRP

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeanza mchakato wa kutathimini mapokeo na matumizi ya teknolojia za kilimo kupitia Mradi wa Mifumo Himilivu ya Chakula (TFSRP). Hatua hii inahusisha mafunzo elekezi kwa watafiti 57. Mafunzo hayo ya siku tatu yalifanyika mkoani Morogoro kuanzia Februari 19–21, 2026, yakijikita katika kujengeana uwezo wa ukusanyaji wa takwimu kwa kutumia teknolojia za kidijitali.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, alisema taasisi ina imani kubwa na watafiti hao na ana matumaini kwamba watafanya kazi yenye tija itakayosaidia kubainisha hali ya matumizi ya teknolojia mbalimbali. Hatua hiyo, aliongeza, inalenga pia kutathmini manufaa ya teknolojia hizo kwa wakulima na kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani wa kilimo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti na Ubunifu, Dkt. Deusdedith Mbanzibwa, alisema tangu mwaka 2021 TARI imesambaza jumla ya teknolojia 121 za kilimo kwa wadau mbalimbali.



Naye Meneja wa Kitengo cha Sayansi ya Jamii na Utafiti wa Masoko, Dkt. George Sonda, alisema ukusanyaji wa takwimu utafanyika kwa awamu mbili. Ambapo awamu ya kwanza ikihusisha mazao ya kimkakati na himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo mpunga, mahindi, mtama, mihogo, viazi vitamu, maharage, karanga na mboga mboga hasa mchicha.

Katika kuwajengea uwezo watafiti, Mwezeshaji wa mafunzo kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) Dkt. Munguatosha Ngomuo alieleza mbinu zitakazo tumika katika ukusanyaji wa takwimu ni pamoja na mahojiano ya ana kwa ana katika kaya za wakulima, majadiliano ya makundi lengwa na ukusanyaji wa sampuli za mimea kwa lengo la uchunguzi wa vinasaba (DNA fingerprinting).

Aidha, katika zoezi hilo la ukusanyaji wa takwimu kwa ushirikiano na maafisa ugani na mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya kaya 2,797 za wakulima katika mikoa 13 ya Tanzania Bara zimefikiwa na watafiti hao ambapo takwimu zilizokusanywa zilihusisha uelewa wa teknolojia za kilimo zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi, kiwango cha mapokeo cha kuridhishwa kwa teknolojia hizo na Kiwango cha matumizi yake.

Kutokana na utafiti huo, baadhi ya matokeo yameonyesha kuwa uelewa wa teknolojia za kilimo zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi ni mkubwa (asilimia 72) lakini kiwango cha upokeaji wake kinatofautiana sana kati ya mkoa mmoja na mwingine. Idadi ya kaya zinazotumia teknolojia kuhusu mbinu rafiki kwa mazingira na zinazo stahimili mabadiliko ya tabianchi ni kaya 222,690 pamoja na kukuza majukwaa ya kujifunza kati ya mikoa na wilaya na kuoanisha mikakati ya usambazaji wa teknolojia hizo ili kupunguza tofauti za mapokeo ya teknolojia za kilimo zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi.



# WATEKELEZAJI WA MRADI WA BRAINS KUTOKA NCHI 15 WATEMBELEA KITUO CHA TARI SELIAN

**UJUMBE** wa watafiti kutoka Taasisi za Utafiti wa Kilimo (NARS) kutoka nchi 15, ukijumuisha Kituo cha Kimataifa cha Fiziolojia na Ikolojia ya Wadudu (ICIPE) pamoja na CIAT, umetembelea Kituo cha TARI Selian na CIAT Tanzania kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa chini ya mradi wa BRAINS unaolenga kujenga ustahimilivu wa kilimo dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Ziara hii imelenga kujifunza na kubadilishana uzoefu juu ya uboreshaji wa mbegu bora za maharagwe, ambapo watafiti wa Kituo cha TARI Selian walionesha mafanikio makubwa katika kubuni aina zinazostahimili hali ngumu za mazingira na kuongeza tija katika uzalishaji.

Kiongozi wa msafara huo, Dkt. Subramanian Seygan, alipongeza kazi kubwa inayofanywa na watafiti wetu na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kuimarisha usalama wa chakula.

Mradi wa BRAINS unaotekelezwa na Kituo cha TARI Selian, TARI Tengeru, ICIPE pamoja na CIAT, chini ya ufadhili wa Bill & Melinda Gates Foundation unaendelea kuleta mageuzi chanya katika sekta za maharagwe, matunda na wadudu.





# TARI, AL SHAHBANDAR KUSHIRIKIANA KUKUZA SEKTA YA MBEGU NCHINI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeeleza dhamira yake ya kushirikiana na Kampuni ya Al Shahbandar ya nchini Misri katika kuimarisha na kukuza sekta ya mbegu nchini, kufuatia mazungumzo yaliyofanyika katika Makao Makuu ya TARI Jijini Dodoma mnamo Februari 9, 2026.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, alisema Taasisi hiyo ina fursa kubwa ya kushirikiana na wadau wa kimataifa kutokana na maono yanayofanana, uzoefu wa pamoja na uwepo wa kampuni zilizojengeka vizuri zinazoweza kuingia katika ushirikiano wa kimkakati. Aidha, alipendekeza kuanzishwa kwa kikosi kazi cha pamoja kitakachojumuisha wataalamu kutoka pande zote mbili ili kuratibu utekelezaji wa ushirikiano huo.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Al Shahbandar, Bw. Khaled Ahmed Fayez, alieleza nia ya kampuni hiyo kujenga ushirikiano wa karibu na TARI, akibainisha kuwa kuunganisha nguvu kwa pamoja ni muhimu katika kuendeleza sekta ya kilimo katika mataifa hayo mawili rafiki.

Alisema kuwa kinachozikutanisha nchi hizo si historia pekee, bali pia uhalisia wa kiuchumi na kijamii, kwani kilimo na sekta ya vijijini ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hizo, zikichangia takribani asilimia 67 ya maisha ya wananchi.



Aliongeza kuwa Kampuni ya Al Shahbandar imechagua Tanzania kutokana na uwepo wa ardhi yenye rutuba, upatikanaji wa maji ya kutosha na mazingira rafiki kwa kilimo, huku akiahidi kufanya kazi bega kwa bega na TARI kuziba pengo la upungufu wa mbegu nchini, linalokadiriwa kufikia tani 50,000 kwa mwaka.

Baada ya majadiliano, kikao hicho kiliazimia kuunda kikosi kazi cha pamoja kitakachojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili, pamoja na kuainisha mpango kazi wa pamoja, majukumu ya kila upande, rasilimali fedha, kukamilisha makubaliano na kuingia mkataba rasmi wa ushirikiano. Pia walikubaliana kuanza uzalishaji wa mbegu za mazao ya alizeti na mahindi.

Ujumbe wa Kampuni ya Al Shahbandar ulijumuisha Dkt. Hossam Awad, Mshauri Elekezi wa Mawasiliano na Maendeleo ya Biashara; Dkt. Abdulnabi Diabi, Mshauri Elekezi na Mtafiti wa Mbegu; pamoja na Dkt. Mohamed Alghunemi, Mshauri Elekezi na Mtafiti wa Mbegu.

Kwa upande wa TARI, ujumbe ulijumuisha Dkt. Sophia Kashenge, Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia na Mahusiano; Dkt. Deusdedith Mbanzibwa, Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu; Dkt. Amachus James, Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Makutopora; Dkt. Atugonza Bilaro Mtafiti Mwandamizi pamoja na watafiti wengine kutoka TARI Makao Makuu na Kituo cha Makutopora.

Ziara hiyo ilihitimishwa kwa ujumbe wa Al Shahbandar kutembelea shamba la zabibu, ambapo walipata fursa ya kujionea shughuli za utafiti wa zao hilo pamoja na kazi za uongezaji thamani wa zabibu.



# TARI NA WADAU WA MBEGU WAUNGANA KUTATUA KITENDAWILI CHA MASOKO

**SEKTA** ya mbegu nchini imeingia katika hatua mpya kufuatia ushirikiano wa karibu kati ya Wadau wa Maendeleo, Serikali na Sekta Binafsi wenye lengo la kuhakikisha mkulima hapati tu mbegu, bali anapata mbegu bora na inayokidhi mahitaji ya soko.

Katika mkutano wa siku mbili uliofanyika Februari 12 na 13 katika Ukumbi wa Mount Meru, Jijini Arusha chini ya mradi wa Accelerated Variety Turnover, wadau hao walikubaliana kuondoa pengo lililokuwepo kati ya watafiti na wafanyabiashara wa mazao ili kuharakisha mapinduzi ya kilimo nchini.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dkt. Thomas Bwana, alisema sekta ya kilimo ni muhimili muhimu wa Dira 2050, ikitarajiwa kuchangia hadi asilimia 40 ya Pato la Taifa. Alisisitiza kuwa malengo hayo hayawezi kufikiwa iwapo wakulima wataendelea kutumia mbegu za zamani zisizoendana na mahitaji ya soko.

Dkt. Bwana aliongeza kuwa TARI imejipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, ambapo mwaka 2025 pekee taasisi hiyo imezalisha tani 125 za mbegu daraja la msingi ili kupunguza upungufu wa upatikanaji wa mbegu nchini.



Kwa upande wake, Dkt. Chris Ojiewo kutoka Kituo cha kimataifa cha Kuboresha Mahindi na Ngano (CIMMYT) alisema mradi wa ACCELERATE umeundwa kutatua changamoto ya kukosekana kwa uwiano kati ya uzalishaji na soko. Alieleza kuwa hapo awali wafanyabiashara walilalamikia ukosefu wa mbegu bora, huku wazalishaji wakidai kukosa soko la uhakika. Kupitia mfumo mpya, mfanyabiashara amewekwa katikati ya mnyororo wa thamani akiainisha aina ya zao analohitaji, mkulima huzalisha kwa uhakika, na mtafiti hutoa mbegu inayokidhi mahitaji hayo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI), Nyasebwa E. Chimagu, alisema taasisi hiyo imeanza kuhamia katika mifumo ya kidijitali ili kurahisisha huduma. Alieleza kuwa usajili wa mbegu sasa utafanyika kwa njia ya mtandao ili kupunguza urasimu, huku kalenda za kidijitali zikianza kutumika kufuatilia mashamba ya mbegu kote nchini. Aidha, aliongeza kuwa marekebisho ya Sheria ya Mbegu yanaendelea ili kuendana na mabadiliko ya soko.

Kwa upande wa wadau wa maendeleo, Bwana Jean Claude Rubyogo wa Taasisi ya Kimataifa ya Pan-Africa Bean Research Alliance (PABRA) pamoja na Jeffrey Ehlers Gates Foundation walisisitiza kuwa mafanikio ya tafiti za kilimo hayapimwi kwa idadi ya aina mpya za mbegu zilizogunduliwa, bali kwa namna zinavyobadilisha maisha ya wakulima. Walihimiza Serikali kuendelea kuimarisha mfumo wa mbegu za daraja la Kuazimiwa Ubora (QDS) ili kuwafikia wakulima wengi zaidi, hasa wa maeneo ya vijijini.





# SILINDE AAHIDI USHIRIKIANO KATI YA WIZARA YA KILIMO NA STARBUCKS KWENYE ZAO LA KAHAWA

**NAIBU** Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde (Mb), amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu Mkuu wa Rais – Utafiti, Maendeleo na Uendelevu kutoka Kampuni ya Starbucks, kampuni yenye makao yake nchini Marekani, Bw. Roberto Alonso Vega, katika Ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Kilimo, Mtumba jijini Dodoma.

Mazungumzo hayo yaliyofanyika Januari 19, 2026 yalilenga kujadili uwezekano wa kuanzisha ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo na Kampuni ya Starbucks katika kuendeleza zao la kahawa nchini, hususan katika maeneo ya utafiti, uzalishaji mbegu na miche bora pamoja na masoko ya zao hilo.

Katika mazungumzo hayo, Mhe. Silinde amemhakikishia Bw. Vega kuwa Wizara ya Kilimo iko tayari kuingia katika makubaliano ya ushirikiano na Kampuni ya Starbucks siku zijazo, kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la kahawa na kuinua kipato cha wakulima.

Timu ya Wizara ya Kilimo iliyoshiriki mazungumzo hayo ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dkt Thomas Bwana, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania, Bw. Primus Kimaryo pamoja na baadhi ya watumishi kutoka Wizara ya Kilimo, TARI Makao makuu na TARI- TACRI.






*Mkurugenzi Mkuu wa TARI DKT. Thomas Bwana akimkabidhi zawadi Rais wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Shandong cha Nchini China Dkt. Leng Changjian wakati alipotembelea Ofisi za TARI Jijini Dodoma.*





*Baadhi ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) wakiwa katika mafunzo kwa vitendo katika Kituo cha TARI Mikocheni*





*Baadhi ya watafiti wa TARI wakifanya mahojiano na wakulima ili kutathmini utumiaji wa teknolojia za kilimo zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi katika baadhi ya mikoa hapa nchini.*



# NAMNA TARI INAVYOWASAIDIA WAKULIMA WADOGO KATIKA MATUMIZI YA KILIMO CHA USAHIHI (PRECISION AGRICULTURE) NCHINI TANZANIA

**TUNAPOZUNGUMZIA** Kilimo cha Usahihi (Precision agriculture) tunamaanisha mbinu za kisasa za kilimo zinazotumia teknolojia na takwimu za kisayansi ili kuboresha matumizi ya rasilimali, kuongeza tija, na kupunguza gharama na athari za mazingira. Kwa wakulima wa Tanzania, hii inamaanisha kutumia vihisi (sensor) GPS, na uchambuzi wa takwimu ili kupanda, kumwagilia, na kupalilia kwa usahihi kulingana na mahitaji halisi ya udongo na mimea.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ina jukumu kubwa la kuwasaidia wakulima wadogo nchini Tanzania kutumia kilimo cha usahihi ili kuongeza uzalishaji, kupunguza gharama pamoja na kulinda mazingira. Wakulima hao hupatiwa maarifa, teknolojia, na takwimu zinazowawezesha kufanya maamuzi sahihi ya kilimo kwa usahihi zaidi ili kuongeza mavuno na kipato.

Mbali na kufanya utafiti, TARI pia hubuni na kusambaza teknolojia mbalimbali zinazofaa kulingana na wakulima wadogo na maeneo waliyopo. Teknolojia hizo ni mbegu bora zinazostahimili ukame na magonjwa, mbinu za kupima afya ya udongo pamoja na teknolojia za zana za kilimo na umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. Hii huwasaidia wakulima kufanya maamuzi sahihi kulingana na hali halisi ya mashamba yao. Katika nchi kama Israel, umwagiliaji wa matone (drip irrigation) hutumiwa sana kuokoa maji yasipotee bure.

Kilimo hiki cha usahihi kinakuwa kwa kasi duniani, kinabadilisha kilimo kutoka kilimo cha kubahatisha Kwenda kwenye kilimo kinachotumia takwimu na teknolojia, na kinatumika zaidi katika nchi zilizoendelea. Kwa mfano, nchini Marekani zaidi ya 70% ya wakulima hutumia GPS. Kwa Afrika, ingawa teknolojia hii iko nyuma kidogo, lakini kuna fursa kubwa ya kukua na ndio maana TARI imeanza kusambaza mbinu hizi kwa wakulima wadogo.

Kwa upande wa matumizi ya takwimu na ramani za kilimo, TARI imekuwa ikishirikiana na Taasisi za ndani na za Kimataifa katika kutoa ramani za udongo, kutoa ushauri wa wakati sahihi wa kupanda na kuvuna mazao pamoja na kutumia mifumo ya kidijitali ambayo husaidia wakulima kuelewa mwenendo wa hali ya hewa. Kwa mfano, nchi za Marekani na Japan zenyewe zinaongoza kidijitali katika matumizi ya teknolojia za matrekta zenye GPS (auto-steering tractors), roboti za kupalilia na kuvuna pamoja na ndege nyuki (drones) kwa ajili ya ufuatiliaji wa mazao.

Mtafiti Emmanuel Mwenda wa TARI Makao Makuu katika maelezo yake kuhusu kilimo cha usahihi alieleza kuwa TARI inahamasisha wakulima kulima kilimo kinacholenga maeneo maalum (site-specific farming) kwa kutumia mbolea kulingana na mahitaji ya sehemu maalum ya shamba, kupanda mazao kulingana na aina ya udongo na kiasi cha mvua pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya pembejeo hali ambayo itamsaidia mkulima kuongeza tija na kupunguza gharama za uzalishaji.

Daktari Tumaini Mazengo ambaye ni Mhandisi na Mtafiti kiongozi wa Utafiti Uhandisi Kilimo anaeleza kuwa zana ya kupanda ngano na kuweka mbolea (Wheat Seed cum Fertilizer Drill) katika majaribio yake ya awali imeonesha kumsaidia mkulima kuokoa kiasi cha kilogramu 53.9 za mbegu na 58.6 za mbolea, pungufu kutoka kwenye kiasi cha kilogramu 125 na 150 za mbegu na mbolea kwa mfuatano ambao ni wastani wa matumizi kwa sasa katika maeneo mbalimbali.

TARI huwafikia wakulima kupitia mafunzo na huduma za ugani kwa kutoa mafunzo ya moja kwa moja kwa wakulima mashambani, kutoa elimu ya matumizi ya simu za mkononi katika kupata ushauri wa kilimo pamoja na kushirikiana na maafisa ugani kuwafundisha wakulima jinsi ya kutumia teknolojia mpya. Aidha, TARI pia hushirikiana na Sekta binafsi (makampuni ya teknolojia za kilimo, Mashirika ya Kimataifa na Miradi ya Serikali) ambayo husaidia kuleta vifaa na huduma kama kihisi (sensor), ndege nyuki (drone) na programu za kidijitali kwa wakulima.

**Je, nini faida ya kutumia kilimo cha Usahihi?**

Mzee Mwinyichande Mkude (56) ni mkulima wa zao la mahindi kutoka Wilaya ya Kilosa. Kabla ya kupata elimu kutoka TARI, alikuwa akipata mavuno kidogo ya mahindi (gunia 8–10 kwa hekta), alikuwa na matumizi yasiyo sahihi ya mbolea pamoja na kupanda bila kuzingatia nafasi (spacing) na kutegemea zaidi mvua katika umwagiliaji, mvua ambazo hazikuwa na uhakika.

**Nini kilibadilika?**

Kupitia programu za TARI na mafunzo mbalimbali, Mzee Mkude alipata mbegu bora (kupitia mradi wa AVISA, alifundishwa kupima udongo (soil testing –na Kituo cha TARI Mlingano), alitumia kifaa cha kupandia kwa nafasi sahihi (Rafiki Planter) na kufuata kalenda ya kilimo kulingana na takwimu za mvua

**Matokeo**

Mzee Mkude baada ya matumizi ya elimu na teknolojia kutoka TARI, alianza kuona tija katika kilimo chake cha mahindi. Mavuno yaliongezeka hadi gunia 20+ kwa hekta, gharama za mbolea zilipungua (alitumia kwa usahihi) na faida iliongezeka zaidi ya mara mbili hali iliyomfanya kuwa balozi mzuri kwa wakulima wenzake ili nao watumie kilimo cha usahihi.

Kwa mujibu wa Daktari Hildelitha Msita ambaye ni Meneja wa Utafiti na Usimamizi wa Maliasili na Uhandisi Kilimo, kilimo cha usahihi kwa sasa ni mkombozi kwa wakulima wadogo kutokana na faida zake pamoja na tija katika mazao. Anabainisha baadhi ya faida hizo kuwa ni:

1. Kuongezeka kwa mavuno: Kilimo cha kisasa hutumia teknolojia kama ramani za GPS, vihisi (sensors za udongo, na picha za satelaiti ili kubaini upungufu wa virutubisho na kutumia pembejeo pale tu inapohitajika.

2. Kupunguza Gharama: Kwa kupunguza upotevu wa maji, mbolea na viuatilifu, mkulima anaokoa pesa huku akiongeza uzalishaji na tija ya mazao.

3. Uendelevu: Matumizi sahihi ya pembejeo hupunguza athari kwa mazingira, huhifadhi udongo na vyanzo vya maji.

4. Kupunguza hatari: Utambuzi wa mapema wa wadudu, magonjwa, au ukosefu wa maji husaidia mkulima kuchukua hatua kabla tatizo halijaenea katika shamba zima.

5. Faida ya Soko: Ubora na uthabiti wa mazao huongeza nafasi ya kupata masoko yenye bei nzuri.

**Baadhi ya miradi, programu na teknolojia zinazogusa kilimo cha usahihi**

1. Biotechnology & tissue culture



(TARI Mikocheni na Kibaha)

Hii ni sehemu ya kilimo cha Usahihi (precision agriculture ) kupitia usimamizi sahihi wa afya ya mazao . Husaidia kupunguza hasara za mazao na kuboresha ubora wa mazao kwa kutumia teknolojia za molecular diagnostics (kutambua magonjwa mapema) pamoja na Tissue culture (uzalishaji wa miche safi).

2. Teknolojia ya Rafiki Planter (Seed Planting Tool). Hii ni moja ya teknolojia bunifu na rafiki ya TARI yenye uwezo wa kupanda mbegu za mazao ya mahindi, alizeti na pamba kwa nafasi sahihi (spacing precision). Teknolojia hii husaidia kupunguza muda wa kupanda kutoka saa 8 hadi saa 1 kwa hekta

3. Maabara na ramani za udongo (TARI Mlingano). TARI kupitia Kituo cha TARI Mlingano hutengeneza na kutoa ramani za udongo (soil maps) kwa kutumia GIS na kutoa mapendekezo ya mbolea kulingana na eneo. Pia, hufanya upimaji wa rutuba ya udongo na kutoa ushauri wa matumizi sahihi ya mbolea. Hii inawezesha wakulima kutumia pembejeo kwa usahihi mkubwa.

**Hitimisho**

Katika nchi za Afrika, wastani wa 10% - 20% ya wakulima wanafikiwa na teknolojia hizi hasa kupitia miradi. Kwa Tanzania, mwamko wa matumizi ya Kilimo cha usahihi umeanza kuonekana, kupitia TARI wakulima wanapewa mafunzo ya kubadilisha kilimo kutoka kilimo cha mazoea hadi kuwa kilimo cha kisasa.

Kwa wakulima wadogo, kilimo cha kisasa hakihitaji mashine za gharama kubwa, kinaweza kuanza na vifaa rahisi na vya bei nafuu kama programu za simu, vihisi vya udongo (sensor) na ndege nyuki (drone).

Kwa kulenga ufanisi na uendelevu, wakulima wa Tanzania wanaweza kuongeza mavuno, kupunguza gharama na kuimarisha ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia kilimo cha usahihi.

Kwa ufupi, TARI inatekeleza kilimo cha Usahihi ( precision agriculture) kupitia:

•Teknolojia za kupanda kwa usahihi (Rafiki Planter na Seed cum Fertilizer Drill)

•Mifumo ya kidijitali (digital seed systems)

•Ramani na takwimu za udongo (GIS & soil testing)

•Umwagiliaji janja na vifaa vya kisasa (ndege nyuki)


•Bioteknolojia na mbegu bora


Njia hizi zote zitamsaidia mkulima mdogo:


•Kupunguza gharama za uzalishaji

•Kuongeza mavuno


•Kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia takwimu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
PONGEZI
Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania(TARI) tunakupongeza
Prof. Peter Msoffe,
Kwa kuteuliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa Naibu Katibu Mkuu Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula wa Wizara ya Kilimo
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV



WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
Heri ya Miaka
62
YA MAPINDUZI
ZANZIBAR
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunawatakia Watanzania wote Heri ya Maadhimisho ya Miaka 62 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar.
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
7th April
HAPPY
KARUME DAY
ABEID AMANI KARUME
Rais wa kwanza wa Zanzibar
4 Augusti 1905 - 7 Aprili 1972
" Mapinduzi yetu ndio mkombozi wa wanyonge tuyalinde, tuyaenzi na tuyadumishe "
SHEIKH ABEID AMANI KARUME
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
KUELEKEA
SIKU YA WANAWAKE
DUNIANI 8 MACHI 2026
Tunajivunia kuwa na viongozi wanawake
uongozi wenu umechangia mafanikio ya Taasisi
Dkt. Sophia Kashenge ( DTTP )
Dkt. Nessie Lwambano ( CD-TARI Kibaha )
Dkt. Happy Moleli ( CD-TARI Tengeru )
Dkt. Chuwa Carisma ( CD-TARI Selian )
Dkt. Suzan Mbwambo ( CD-TARI TACRI )
Dkt Geradina Mzena ( CD-TARI Naliendele )
Selina Mloge ( HLU )
Ediltruda Maseko ( AM )
Dkt. Hildelitha Msita ( MNRMAER )
Evelyne Mpasha ( MKMC)
Margareth Ndebelamatwi ( Chief Accountant )
Kaulimbiu:
Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana:
Msingi Jumuishi kufika DIRA 2050
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
EiD
al-Fitr
MUBAARAK
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunakutakia heri ya sikukuu ya Eid al Fitr.
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
IJUMAA KUU NJEMA
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunawatakia Wakristo wote Ijumaa Kuu njema.
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HERI YA
SIKUKUU YA
PASAKA
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inawatakia heri ya Sikukuu ya Pasaka Wakristo na Watanzania wote kwa ujumla.
Mathayo 28:6
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
8
MACHI
2026
HERI
YA SIKU
WANAWAKE
DUNIANI
Wanawake ni nguzo ya maendeleo ya kilimo. TARI tunatambua na kuthamini mchango wa wanawake katika kuendeleza sekta ya Kilimo.
"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufika DIRA 2050".
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV




# TARI NALIENDELE YATUMIA MICHEZO KUTANGAZA TEKNOLOJIA

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kupitia Kituo chake cha TARI Naliendele, imeshiriki michezo ya kirafiki na Wakala wa Umeme Tanzania (TEMESA), mnamo tarehe 10 Januari 2026 katika viwanja vya mpira wa miguu vilivyopo katika ofisi za kituo hicho Mkoani Mtwara.

Michezo hiyo ilikuwa na lengo la kuimarisha afya na mahusiano baina ya taasisi hizo mbili, huku ikitumika kama jukwaa la kutangaza teknolojia mpya za kilimo.


Katika mchezo huo wa kirafiki,Kituo cha TARI Naliendele kiliibuka na ushindi wa mabao 3–0 dhidi ya timu ya TEMESA. Akizungumza katika hafla hiyo, Mratibu wa zao la Ufuta, Bw. Joseph Nzunda, alibainisha kuwa michezo hiyo ni daraja la kuunganisha taasisi na wadau mbalimbali wakiwemo madiwani na wananchi.

Nzunda aliongeza kuwa uongezaji thamani wa mazao mbalimbali kama ufuta, akitolea mfano wa bidhaa ya Sesalemo inayotokana na ufuta kuwa bidhaa hiyo ina sifa ya kuimarisha misuli na kutibu matatizo ya ngozi kama miwasho na mapunye.

Kituo cha TARI Naliendele kinaendelea kuwa kitovu cha uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya korosho, karanga na ufuta nchini.




TARI
Transforming Agriculture
UTEUZI NDANI YA TAASISI
Dkt. Mpoki Shimwela ameteuliwa kuwa Meneja wa utafiti wa mazao na usimamizi wa mazao baada ya mavuno TARI Makao Makuu. Anachukua nafasi ya Dkt. Atugonza Bilalo ambaye ana kwenda kuongeza nguvu katika utafiti wa zao la mpunga katika Kituo cha TARI Ifakara. Uteuzi huo umeanza tarehe 19 Februari, 2026.
Dkt. Fredy Tairo ameteuliwa kuwa Meneja wa Maabara ya "Bioscience" TARI Makao Makuu. Uteuzi huo umeanza tarehe 19 Februari, 2026.
Dkt. Khadija Mussa Ally ameteuliwa kuwa Kaimu Meneja wa Kituo cha TARI Mauku. Uteuzi huo umeanza tarehe 19 Februari, 2026.
Bi. Evangelista Chiunga ameteuliwa kuwa Kaimu Meneja wa Kituo cha TARI Mikocheni. Uteuzi huo umeanza tarehe 24 Februari, 2026.
Tuwape Ushirikiano katika kutimiza majukumu yao
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
TANZIA
Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dkt. Thomas Bwana anasikitika kutangaza Kifo cha aliyekuwa Mtafiti Daraja la Kwanza (I) Bw. DADILI JAPHET MAJUME katika Kituo cha TARI Naliendele kilichotokea leo Tarehe 03 Aprili, 2026.
"Bwana ametoa na Bwana ametwaa jina la Bwana Lihimidiwe"
Tufuatilie
Tari Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TariTV

# MAJUKUMU YA UTAFITI KWA VITUO (RESEARCH MANDATES)







| Na. | KITUO | MAJUKUMU YA UTAFITI |
|---|---|---|
| 1. | TARI Uyole - Mbeya | Viazi mviringo, uhandisi kilimo, maharage, mahindi, pareto na mazao ya bustani |
| 2. | TARI Kifyulilo - Iringa | Viazi mviringo, maharage, mahindi, ngano, chai na mazao ya bustani |
| 3. | TARI Ukiriguru - Mwanza | Pamba, mazao ya mizizi na mazao ya bustani |
| 4. | TARI Maruku - Kagera | Migomba, maharage na mazao ya bustani |
| 5. | TARI Selian - Arusha | Maharage, ngano na shayiri, mazao jamii ya mikunde na mazao ya bustani |
| 6. | TARI Tengeru - Arusha | Mazao ya bustani |
| 7. | TARI Naliendele - Mtwara | Mikorosho, mazao ya bustani na mazao ya mafuta (karanga na ufuta) |
| 8. | TARI Ilonga - Morogoro | Mahindi ya Nyanda za chini, mazao jamii ya mikunde, alizeti, mtama, uwele, ulezi, teknolojia ya mazao baada ya mavuno na mazao ya bustani |
| 9. | TARI Dakawa - Morogoro | Mpunga na mazao ya bustani |
| 10. | TARI Ifakara - Morogoro | Mpunga na mazao ya bustani |
| 11. | TARI Tumbi - Tabora | Kilimo misitu (agroforestry) na mazao ya bustani |
| 12. | TARI Mlingano - Tanga | Udongo, mkonge na mazao ya bustani |
| 13. | TARI Kibaha - Pwani | Miwa na mazao ya bustani |
| 14. | TARI Mikocheni – Dar es Salaam | Nazi, bioteknolojia na mazao ya bustani |
| 15. | TARI Makutupora - Dodoma | Zabibu na mazao ya bustani |
| 16. | TARI Hombolo - Dodoma | Mazao himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi: mtama, uwele ulezi na mazao ya bustani |
| 17. | TARI Kihinga - Kigoma | Michikichi na mazao ya bustani |
| 18. | TARI TaCRI - Kilimanjaro | Kahawa na mazao ya bustani |
| 19. | TARI TORITA - Tabora | Tumbaku na mazao ya bustani |
| 20. | TARI TRIT - Iringa | Chai na mazao ya bustani |

**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)**
**S. L. P 1571, Dodoma**
**Tel: +255 26 2961 995/e-mail:dg@tari.go.tz**
**Website:www.tari.go.tz**

TariTanzania | Tanzaniatari | official_ taritanzania | TARI Tanzania | TARI